

Mstari huu una maana gani? “Mathayo 23:39 Hamtaniona kamwe tangu sasa”

SWALI: Mathayo 23:39 “Kwa maana nawaambia, Hamtaniona kamwe tangu sasa, hata mtakaposema, AMEBARIKIWA AJAYE KWA JINA LA BWANA.”

JIBU: Ukisoma kuanzia juu utaona habari hiyo alikuwa anaizungumza Bwana Yesu alipokuwa anaingia Yerusalemu, Na kuona jinsi mji ule ulivyo mkataa, na kukataa wokovu tangu zamani za Manabii wa agano la kale hadi wakati wake, Na jinsi ulivyowaua wale wajumbe wote waliotumwa kwake,..Ndipo hapa sasa Yesu akautabiria kuwa atauacha katika hali ya ukiwa mpaka hapo watakapogeuka..

Embu tusome..

Mathayo 23:37 “Ee Yerusalemu, Yerusalemu, uwauaye manabii, na kuwapiga kwa mawe wale waliotumwa kwako! Ni mara ngapi nimetaka kuwakusanya pamoja watoto wako, kama vile kuku avikusanyavyo pamoja vifaranga vyake chini ya mabawa yake, lakini hamkutaka!

38 Angalieni, nyumba yenu mmeachiwa hali ya ukiwa.

39 Kwa maana nawaambia, Hamtaniona kamwe tangu sasa, hata mtakaposema, Amebarikiwa ajaye kwa jina la Bwana”.

Unaona, Na historia inaonyesha kweli, Wayahudi waliachwa na Mungu, tangu huo wakati hadi sasa ni miaka 2000 imeshapita, bado hajawarudiwa na mji wa Yerusalemu nao ulikuwa ni magofu tangu zamani, ni karne za juzi juzi tu ndio umeanza kujengwa tena na kukaliwa na watu.., lakini Bwana hakuishia tu pale, bali alisema, utaendelea kuwa hivyo hivyo katika hali ya ukiwa mpaka siku hiyo watakaposema tena Amebarikiwa ajaye kwa jina la Bwana..Yaani ikiwa na maana watakapotubu na kumtambua Kristo kuwa ni yule masihi kweli..

Lakini ni kwanini aseme “hata mtakaposema, AMEBARIKIWA AJAYE
KWA JINA LA BWANA.” Na si mpaka hapo mtakaposema mimi ni
Masihi?

Utakumbuka tukio lililotendekeza nyuma kidogo kabla hajafika
Yerusalemu alikuwa anaimbiwa hayo maneno Hosana, Hosana
Amebarikiwa ajaye kwa jina la Bwana...

Na ndio maaana utaona Bwana akitumia maneno hayo hayo tena
kuashiria kuwa mpaka siku wayahudi watakapompokea yeye kwa namna
hiyo hiyo, ndipo wokovu utageuka kwao. Na dalili zote zimeshaanza
kuonekana sasa, Israeli imeshakuwa taifa huru, wayahudi wanaanza
kuyagundua makosa yao kidogo kidogo..Je! Unadhani ni kitu gani
kitatokea muda mfupi baadaye.. Bila shaka watamgeukia na kutubu..Na
biblia inasema siku watakapomgeukia uovu wao utaondolewa wote
ndani ya siku moja..

Kama unabii inavyosema..

Zekaria 12:10 “Nami nitawamwagia watu wa nyumba ya Daudi, na wenyeji wa Yerusalemu, roho ya neema na kuomba; nao watamtazama yeye ambaye walimchoma; nao watamwombolezea, kama vile mtu amwombolezeavyo mwanawe wa pekee; nao wataona uchungu kwa ajili yake, kama vile mtu aonavyo uchungu kwa ajili ya mzaliwa wake wa kwanza.

11 Siku hiyo kutakuwa na maombolezo makuu huko Yerusalemu, kama maombolezo ya Hadadrimoni katika bonde la Megido.

12 Nayo nchi itaomboleza, kila jamaa peke yake; jamaa ya nyumba ya Daudi peke yao, na wake zao peke yao; jamaa ya nyumba ya Nathani peke yao, na wake zao peke yao;

13 jamaa ya nyumba ya Lawi peke yao, na wake zao peke yao; jamaa ya nyumba ya Shimei peke yao, na wake zao peke yao.

14 Jamaa zote zilizosalia, kila jamaa peke yake, na wake zao peke yao”.

Sasa tukishaona mambo hayo yanatokea, basi ujue kuwa Neema ya wokovu imeshaondoka kwetu, na Unyakuo tayari umeshapita.

Mstari huu una maana gani? “Mathayo 23:39 Hamtaniona kamwe tangu sasa”

Ni nyakati za mwisho tunazoishi, Je, bado na wewe upo vuguvugu? Unataka na wewe uachwe ukiwa kwa mfano wa Wayahudi walivyoachwa zamani kwa kutokutubu kwao? Wakati ambao utamtafuta Bwana hutamwona, utautafuta wokovu hutaupata?. Usitamani kabisa wakati huo ukukute hali bado upo dhambini, tubu, itii injili inapohubiriwa kwako kila siku,..UNYAKUO upo mlangoni.

Maran atha!.

Tafadhali washirikishe na wengine habari hizi njema, na pia kama utapenda tuwe tunakutumia masomo haya kwa njia ya email yako au Whatsapp tutumie ujumbe kwenye box la maoni chini au piga namba hii +255 789001312

Mada Nyinginezo:

MAOMBI YA VITA

Mstari huu una maana gani? “Mathayo 23:39 Hamtaniona kamwe
tangu sasa”

*WATAMTAZAMA YEYE AMBAYE WALIMCHOMA; NAO
WATAMWOMBOLEZEA.*

BUSTANI YA NEEMA.

UMUHIMU WA KUZALIWA MARA YA PILI.

JE! UMEBATIZWA UBATIZO SAHIHI?

Mstari huu una maana gani? “Mathayo 23:39 Hamtaniona kamwe
tangu sasa”

Rudi Nyumbani:

Share on:
WhatsApp

[Print this post](#)